

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram "AFYA", DODOMA
Namabari ya Simu: +255 026 – 2323267



Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya
S.L.P. 743,
40478 DODOMA.

**TAARIFA YA SERIKALI KWA UMMA KUHUSU MASWALA MBALIMBALI
YANAYOHUSU MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA CORONA (COVID-19)**

**SWALA LA 1. UFAFANUZI KUHUSU UVUMI WA KUTUMIKA DAWA ZA KAWAIDA
KATIKA KUKINGA AU KUTIBU UGONJWA WA CORONA**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inapenda kutoa ufafanuzi kuhusu uvumi unaoendelea kutolewa na baadhi ya watu juu ya dawa zinazoweza kutumika kutibu au kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa Corona hapa nchini.

Hivi karibuni, kumekuwa na taarifa za uvumi huu katika mitandao ya kijamii kuhusu dawa mbalimbali zinazoweza kutibu au kuzuia ugonjwa wa Corona. Hii imepelekea baadhi ya dawa za kutibu magonjwa tuliyoyazoea kutumika kiholela miongoni mwa wananchi wetu. Aidha, taarifa hizo zinadai kuwa dawa kama Azithromycin, Aspirin, Prednisolone, Zinc, Ascorbic Acid (Vitamin C) na baadhi ya Dawa za Ukimwi (ARV) zinaweza kuzuia au kutibu ugonjwa wa Corona.

Wizara inapenda kuufahamisha Umma kuwa mpaka sasa **HAKUNA DAWA YA KUZUIA AU KUTIBU CORONA**. Dawa zote hutumika kwa kuzingatia mwongozo wa Daktari. Dawa kama Azithromycin hutumika kutibu magonjwa mbalimbali kama magonjwa ya homa ya mapafu itokanayo na bacteria na siyo Virus. Dawa ya Aspirin hutumika kwa ajili ya maumivu, homa na wagonjwa wa moyo kwa maelekezo maalumu ya Daktari, Prednisolone kwa magonjwa kama ya Ngozi, Pumu n.k na Dawa za ARV kwa ajili ya wagonjwa wenye virusi vya UKIMWI.

Matumizi ya kiholela ya dawa hizi yanaweza kusababisha madhara makubwa ikiwemo usugu wa dawa (Resistance) na hivyo kushindwa kutibu tena magonjwa yanayotokana na bakteria. Dawa zingine zina madhara makubwa mfano Aspirini huweza kuleta vidonda vya tumbo na kutokwa na damu, na Prednisolone huweza kuleta madhara ya kupandisha sukari na kuvimba baadhi ya sehemu mwili mzima. Aidha, dawa zingine kama Ascorbic Acid (Vitamin C) na Zinc, ni virutubisho ambavyo vipo kwenye matunda mbalimbali nchini na hutumika tu kama mbadala wakati mgonjwa anayeumwa hawezi kula matunda kwa kiwango kinachotakiwa. Kama hizi dawa zingelikuwa zinatibu au kuzuia hili tatizo basi, vingelikuwa vimeshatumika sana huko Uchina, Ulaya na Marekani maana huko ndo zinazalishwa kwa wingi.

Wizara inawasihi wananchi kupuuza taarifa zisizo za kweli na hivyo kutakiwa kuisikiliza Wizara kupata taarifa sahihi na zenye ushahidi. Wizara inasisitiza kuwa;

1. Hadi sasa hakuna dawa ya kutibu au kuzuia ugonjwa huu, ila kuna dawa zinazoweza kusaidia kutibu mgonjwa akiwa katika hatua fulani, kwa ushauri wa daktari
2. Hakuna uthibitisho wa dawa hizi kuwa zinaweza kuzuia au kutibu Corona
3. Dawa zote lazima ziandikwe na Daktari na si kila mtu atumie kwa jinsi anavyojisikia.
4. Wananchi wanaojihisi dalili zozote za ugonjwa wa COVID-19 wanashauriwa kutoa taarifa kwa kupiga simu namba 199 bila malipo.
5. Baraza la Famasia lisimamie kikamilifu uuzwaji holela wa dawa hizi katika maduka ya Dawa ili kuzuia usugu wa dawa kwa watanzania.

SWALA LA 2, KUHUSU TAARIFA YA TIBA ASILI/MBADALA ZA MITISHAMBA.


Serikali kupitia Wizara hii inaelekeza vyombo vyake hasa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya binadamu, Kitengo cha Wizara cha Tiba Asili/Tiba Mbadala na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba Muhimbili. Kwa pamoja zitolee ufafanuzi na Elimu kwa jamii kuhusiana na Tiba Asili/Mbadala na njia za Kufukizia au Kunywa.

Aidha, Serikali yetu kupitia Wizara ya afya itaendela kutoa maelezo na ufafanuzi wa matibabu ya ugonjwa CORONA kutokana na Tafiti au Ushahidi kamili kadili unavyoendelea kupatikana.

SWALA LA 3, WIZARA INAELEKEZA HAKUNA SABABU YA MAITI ZA WAPENDWA WETU WALIOFARIKI KWA UGONJWA WOWOTE ULE, KUZIKWA USIKU AU GIZANI katika kipindi hiki. Tunaelekeza maafisa Afya na waganga wakuu wa wilaya na mikoa kuhakikisha familia zinashirikishwa kikamilifu na bila hofu au haraka katika kuandaa na kufanya mazishi kwa heshima zote za utu.

Mwisho, Wizara inaendelea kuisisitiza Wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na Ugonjwa huu kama ilivyoelekezwa wa watalaamu wetu.

Imetolewa na:



Prof. Abel Makubi

Mganga Mkuu wa Serikali

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Dar es Salaam, 3 Mei 2020